

WAJUMBE WA

MATUMAINI

COVID-19

Ni mada zipi zinazokosekana kulingana na simu kwa Shirika Kuu La Imani / Viongozi wa Jamii wa Imani kutoka kwa nchi 8?

- **Uhai** – sio kifo; lengo katika COVID-19 lazima libadilike liwe kuendelea kuishi
- **Matumaini** – hakuna uoga; kuwa mbali na wengine hupunguza kuenea kwa COVID-19
- **Muunganisho** – hakuna kujitenga; simu, ujumbe, WhatsApp, kwa walio karantini
- **Mfano Mwema**– uzuiaji wa kawaida, jiepushe na mikusanyiko mikubwa
- **Kujali** – kwa usalama; kwa walioathiriwa na COVID-19, katika nyumba zetu, mikutano, na jamii
- **Sherehe** – sio fedheha; kwa wanaopata nafuu, waliopona
- **Ushawishi** – hujenga tumaini, shukrani, huruma; kwa kuwa viongozi wa imani wanaweza kutumia maubiri ya mtandaoni/ mikutano, ujumbe/radio/Runinga

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na Susan Hillis shillis@cdc.org



UHAI

- Tunaweza kuwa na matumaini ya kweli katika kuwepo kwa COVID-19 Visa vingi vya COVID-19 huwa sio vikali; watu wengi wanaopata COVID-19 hupona; na kila mtu anaweza kuchangia katika kuzuia visa vipya kwa kuchukua hatua rahisi kama kukaa mbali na wengine, usafi wa mikono, kufunika mdomo na pua unapokohoa au kupiga chafya, kuvaa barakoa na kujiepusha na mikusanyiko ya watu.
- Uhai ni zawadi kutoka kwa Mungu ambayo tuna faida ya kushiriki, kulinda na kusherehekea na kwa dada na ndugu.



UHAI

- COVID-19 inaweza kushindwa asante kwa juhudi zetu za pamoja – ili tuweze kuwa na uhai ulio tele: nawa mikono yako mara kwa mara; kohoa au upige chafya kwenye kiwiko chako kilichokunjwa; jiepushe na kugusa macho, pua na mdomo wako; zuia mikutano ya kijamii na muda unaotumika katika maeneo yenye umati; na, unapokuwa na wengine, vaa barakoa!
- Hatua za kushangaza za huruma zinaendelea ulimwenguni kote ili kuzuia kuenea kwa COVID-19 Kuza maisha!
- Tunaweza kuungana pamoja dhidi ya vurugu na unyanyasaji wakati wa COVID-19!



UHAI



- Nena neno la huruma na kutia moyo kwa watoto wako. Wamekuwa mashujaa katika nyakati hizi!
- Uhai wako ni muhimu! Ulinde: nawa mikono yako; vaa barakoa; jiepushe na mahali palipo na umati; chungu umbali wako na watu!
- Maisha ni zawadi ya thamani; yashughulikie hivyo – tunajilinda wenyewe na watu wa jamii ya imani yetu kutokana na COVID-19 kwa kuvaa barakoa; kuzoea kunawa mikono mara kwa mara na kukaa mbali na wengine; na kujiepusha na mikusanyiko mikubwa ya watu.
- Hebu tuzungumze kinyume na vurugu na unyanyasaji katika jamii zetu za imani. Uhai ni zawadi kutika kwa Mungu.

MATUMAINI



FAITH AND COMMUNITY INITIATIVE

- Kuwapa watu matumaini ni jukumu langu kama kiongozi wa imani. Pamoja, tunaweza kushinda COVID-19 ! OU Kuwapa watu matumaini ni jukumu kuu la viongozi wa imani na jamii ya imani. Pamoja tunaweza kushinda COVID-19.
- Kwa kuzifuata hatua zilizopendekezwa kama umbali wa kimwili, kunawa mikono na kuvaa barakoa, pamoja tunaweza kuzuia kuenea kwa COVID-19!
- Pamoja, tunaweza kushinda COVID-19!
- Matumaini yangu, ukweli, kuweza kuhisi maono ya mwingine na huruma vinasalia kuwa miamba yetu imara.
- Katikati ya maumivu tunayoendelea kuvumilia, tunaweza kupata faraja katika hadithi za matumaini na umoja, na tunaendelea kuona thamani katika masomo mema, ya kutia moyo yanayoibuka.

MATUMAINI

- Katika kukabiliwa na changamoto yoyote, tunasimama – katika huruma, matumaini na upendo.
- Kuwa na nguvu, ujasiri na uwe na matumaini! Makumi ya maelfu ya wanasayansi wanafanya kazi kila saa; watafiti wanatafuta njia bunifu za kutoa mchango wa wakati, bidhaa na taaluma zao ili kushinda COVID-19.
- Utafutaji wa chanjo ya COVID-19 umezileta pamoja jamii za sayari za kisayansi na kimatibabu katika njia zisizowahi kufanyika. Hebu tuungane kwa maombi kuzisaidia juhudi zao!
- Katika wakati wa COVID-19, ni roho ya umoja wa kiulimwengu ambayo hutupa matumaini – COVID-19 itashindwa mara watu, katika nchi zote, wanapolindwa – kupitia hatua zetu za pamoja - kutoka kwa virusi vya korona.



MATUMAINI

- Kwa sauti ya matumaini na hekima katika nyakati hizi za changamoto – Shiriki taarifa sahihi kuhusu COVID-19 katika jamii yako ya imani. AU Ningependa kuwa sauti ya hekima katika nyakati hizi zenye changamoto. Ninashiriki taarifa ya kisayansi inayozingatia ushahidi kuhusu COVID-19 katika jamii yangu ya imani.
- Kuwa mjumbe wa matumaini na umoja katika jamii yako ya imani AU Mimi ni mjumbe wa matumanini na umoja katika jamii yangu ya imani.
- Kuwa Mwerevu. Tambua ndoto zako– fuata hatua zilizopendekezwa kama kunawa mikono mara kwa mara na kuvaa barakoa – ili kujilinda na kuwalinda unaowapenda kutokana na COVID-19 AU Ningependa kuzitambua ndoto zangu hivyo ninajilinda mimi mwenyewe na ninaowapenda kutokana na COVID-19 nikizifuata hatua zilizopendekezwa kama kunawa mikono mara kwa mara na kuvaa barakoa.
- Matumaini: Ubiri ujumbe wa matumaini!



KUJUMUIKA



- Mungu yuko kila mahali, Hayuko karantini!
- Sote tunaweza kuwa mbali na kila mmoja NA kujumuika kijamii– kwa kutumia simu, dijitali na chaguo za mbali.
- Ikiwa utahisi kuwa peke yako, wasiliana na sisi: katika jamii yetu ya imani tumeweka kikundi cha usaidizi ambapo watu wanaweza kushiriki changamoto zao na, pamoja, tutambue baadhi ya suluhisho ili kusaidiana.
- Hebu tupange njia za wanajamii kuwafikia wale wanaoishi peke yao au wanaoweza kuwa na hitaji la chakula, maji, au bidhaa zingine.
- Katika wakati wa COVID-19, ni roho ya umoja wa kiulimwengu ambayo hutupa matumaini – COVID-19 itashindwa mara watu, katika nchi zote, wanapolindwa – kupitia hatua zetu za pamoja - kutoka kwa virusi vya korona.
- Tuko kwa hili pamoja, lakini lazima tukae kando. Tafadhali acha nafasi kati yako na wengine.



MIFANO BORA

- Ongoza kwa kuwa mfano ! Wahimiza watu wa jamii kuwa mfano mwema kwa familia zao, marafiki, na jamii yao kwa kufuata ushauri kuhusu COVID-19 kutoka kwa madaktari, mamlaka ya afya ya eneo, na serikali.
- Mimi huwahimiza watoto wangu kuzizoea tabia nzuri kupitia nyimbo na densi – Hii inawasaidia kuhisi wakiwa salama zaidi; kuelewa vyema zaidi jinsi hatua yao ni muhimu katika kuzuia kuenea kwa COVID-19; na kujifunza muunganisho wa maana ni nini.
- Sisi Viongozi wa Imana wa Vijana tunasimama imara kwa afya: tunyajali makundi yaliyo hatarini katika jamii yetu kwa kunawa mikono yetu, kuvaa barakoa na kukaa mbali na wengine.
- Wanaume wa nguvu ni mifano bora. Tunapozifuata ndoto zetu kwa ajili yetu wenyewe, familia zetu, jamii yetu ya imani, taifa letu, tunazifuata hatua zote zinazohitajika ili kupunguza kuenea kwa COVID-19.
- Penda jirani yako unavyojipenda! Walinde walio katika hatari katika jamii yako kwa kunawa mikono yako, kuvaa barakoa na kukaa mbali na wengine.



KUJALI

- Sote tunapaswa kukaa tukijua hatari za COVID-19 ili tuweze kulindana na kutunzana.
- Penda jirani yako kama unavyojipenda! Kwa kuheshimu mipango ya serikali ya kuzuia kuenea kwa COVID-19, tunawapenda majirani wetu kama afanyavyo Mungu.
 - Usisahau: kwa kuyafuata mapendekezo na mikakati ya kujilinda, kuwalinda tuwapendao na kuilinda jamii yetu kutokana na COVID-19, tunawasaidia wale wanaofanya kazi katika mstari wa mbele kama vile wauguzi na madaktari kuwasaidia kwa njia bora zaidi watu wanaohitaji utunzaji.
 - Ninaposhiriki katika kuwatembelea wagonjwa, huhakikisha kuwa nimenawa mikono yangu kabla na baada ya ziara, na kukaa mbali na wengine, hata ninapowaombea wengine. Mwongozo wa kitaifa wa kufunika uso ni muhimu na ni lazima sote tuufuate!
 - Kuwajali wengine humaanisha kujiepusha na mikusanyiko ya watu! Tumia vyombo vya habari na vifaa vya teknolojia ya kisasa kukusanyika katika maombi. Hata pasipo kuwa pamoja kimwili, unaweza kujiunga na wengine katika ushirika wa maombi.



- Hakuna hatua iliyo ndogo sana: Ongoza kwa kuwa mfano –vaa barakoa; kaa mbali na wengine; nawa mikono yako; na UOMBE!
- Wafikie ili kuonyesha huruma kwa wengine wakati wa nyakati za kufungiwa na kuzuiwa kutembea.
- Kuwa kifaa cha uwepo wa Mungu katika watu ambao wanateseka kwa sababu ya COVID-9. Waruhusu kuhisi mguso wa uponyaji wa Mungu kupitia utunzaji wetu wa huruma.
- Sote tunapaswa kutenga muda wa kukaa na watoto wetu: watauthamini katika maisha yao yote, kama tutakavyofanya kila mmoja wetu sisi viongozi na wazazi.
- Mimi huvaa barakoa, kama kitendo cha UPENDO, ili kuwalinda wazee katika jamii ambao hasa wako katika hatari.



SHEREHE

- Katika jamii yetu ya imani tunakaribisha na kuwasherehekea wahudumu wa afya na watu waliopona kutokana na COVID-19.
- Uhai ni zawadi ya thamana ya Mungu na tumeheshimika kuwa na watu waliopona kutokana na COVID-19 kama wanachama wa jamii yetu ya imani!
- Tunasherehekea afya katika mwili na nafsi za wale wote waliopona kutoka na COVID-19.
- Tunasherehekea afya yako na uonyaji kutokana na COVID 19!
- Tunawasherehekea wafanyakazi wote wa mstari wa mbele!
- Tunashiriki huruma na upendo kwa wale walio wagonjwa: ni watoto wa Mungu wanaopaswa kusherehekewa. KAMWE usiwahi kufedheheshwa.



SHEREHE

- (Sisi) Hushiriki hadithi maridadi za wahudumu wa afya, watu waliojitolea, na watu ambao wanapona tokana na COVID-19.
- Kunazo ishara thabiti zaidi kila wakati za matumaini na umoja, hali ya, na hamu ya umoja– Lazima hizi zisherehekewe! Shiriki hadithi zako za matumaini!
- Uhai ni zawadi ya thamani kutoka kwa Mungu. Tumia kila fursa kuthamini maisha ya wale waliopona lutokana na COVID-19.



USHAWISHI

Sisi viongozi wa imani tunashiriki ujumbe wa uzuiaji ili kuzuia kuenea kwa COVID-19 Hebu tuishi, tutumaini, tuunganike, tujali na tusherehekea pamoja!!!

Ongoza ukiwa kweneye mstari wa mbele!

